# Jinsi ya kuwatunza Nyuki



**Wafuga nyuki wanaukagua mzinga wa vito vya juu (top bar)**

Picha za ziada zimetolewa na Mike Brown, Brian Durk na Claire Waring

# MPANGILIO WA KAZI

**Zuru bustni ya nyuki mara kwa mara. Fanya tu jambo moja kwa kila safari, na hakikisha kazi hiyo inalingana na msimu wa mwaka. Ifuatayo ni mifano:**

1. **Fanya usafi karibu na mizinga na hakikisha mizinga imeotewa na ni salama.**

2. **Kagua ndani ya mizinga na kuona kama:**

- **Nyuki wajenga sega sawa sawa (kila sega kwa kila ufito wa juu);**
- **Nyuki malkia anatumikia visawa sawa;**
- **Hakuna maji yanayovuja;**
- **Hakuna mavazi kama vile mchwa, *beetles* au buibui**
- **Hakuna magonjwa yanayowadhuru nyuki.**

3. **Vuna asali:**

- **Vuna tu asali iliyokomaa;**
- **Usivivune vyana vya nyuki;**
- **Usiwaue nyuki;**
- **Bakisha asali kidogo kwa chakula chao nyuki.**

4. **Baada ya kuvuna:**

- **Ondoa nje masega zilizo nje na matupu;**
- **Pangilia sega kwa kuhakikisha hakuna mianya;**
- **Wabakishie nyuki asali kidogo;**
- **Walishe nyuki kama itabidi au inapohitajika.**

5. **Ikiwa nyuki watausia mzinga:**

- **Vuna sega zote ili kunyakua nta;**
- **Safisha uchafu na vijani kutoka kwenye mzinga;**
- **Tumia moto kuwamaliza wadudu wowote waharibifu au dhidi ya magonjwa;**
- **Tia nta kwa fito za juu upya na kuzirudisha kwenye mzinga ulio safi.**

# SEHEMU HII ITAKUSAIDIA KUUKAGUA MZINGA KWA USALAMA NA KUELEWA UNACHOKIONA

1. **Vaa mavazi yanayokinga.**



**Kivizio.**

**Sehemu ya juu ya sare ya nyuki.**

**Mifuko ya mikono.**

**Suruali ndefu ya sare.**

**Tumia buti za matope au mifuko ya mpira (Jwala) kwenye miguu iliofungwa kwenye kifundo cha miguu.**

2. **Hakikisha vifaa vyako vyote viko tayari. Ni vizuri kumhusisha rafiki kusaidia.**



3. **Washa kifukio ili kuwa na moshi wa taratibu. Makoba ya mahindi, nyasi iliokauka na miti iliooza vyote vinafaa kwa kufukia moshi.**






4. **Fukia moshi kwenye lango vizuri na ungojee nyuki wasite.**



5. **Fukia chini ya paa la mzinga vizuri kisha uinue paa.**



**6. Chunguza kwanza sehemu nyuki walioabiria (kwa kugonga gonga). Mlio mwepesi unaashiria sehemu uliotupu mzingani.**




**7. Kwa utararitu inua ufito wa kwanza wa juu.**




**8. Agua kwa upole usega unaofuata ili kuwe rahisi na huru kutolewa.**



**9. Inua kila usega nje kabisa kwa utaratibu ili kuweza kuukagua.**



**Hapa wafuga nyuki wanawakagua nyuki watumwa na nyuki malkia kuhakikisha kwamba kiota kinajengeka sawa sawa.**

**10. Songesha tu usega mmoja mmoja kwa wakati.**



**11. Tazama jinsi muundo huu wa usega wa mwituni ulivyofanana na muundo wa usega wa mzinga wa kisasa wa top bar.**



**12. Nyuki watumwa hawa wanatia asali na mbelewele.**




**13. Nyuki watumwa hawa wanaanzishia usega mpya wa nta.**




**14. Mzinga huu umefurika zaidi na unahitaji kuvunwa.**



**15. Nyuki hawa watumwa wanalinda vyana vya nyuki kabla ya kuangua. Unaweza, kwa kutazama, kutambua vyana vilivyoziba, ambavyo havijaziba, nyuki watumwa au mbelewele kwenye picha hii?**




**16. Nyuki hawa wa ugonjwa mbaya na wanafaa kuharibiwa kwa kuchoma usega.**




**Kiota kilichozama kieusi.**

**Uwekezaji mbaya wa vyana.**

**Nyuki hawa wana viota vilivyohadhirika na ukombo kombo.**